

## **MRADI WA KUNUSURU KAYA MASIKINI TASAF**

### **UTANGULIZI**

Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya ni miongoni mwa Halmashauri saba (7) zinazotekeleza mpango wa kunusuru kaya masikini katika mkoa wa Mbeya. Katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya Mpango huu ulianza kutekelezwa Julai 2015, baada ya wawezeshaji kutoka TASAF Makao Makuu kuutambulisha mpango kwa wadau wakiwemo waheshimiwa madiwani, Mh. Mbunge, wakuu wa idara na wawezeshaji 70 kutoka ngazi ya kata.

Mpango wa TASAF katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya unatekelezwa katika vijiji 105 kati ya vijiji 152. Jumla ya kaya 10,325 zinanufaika na mpango huu ambapo mpaka sasa jumla ya Tsh. 3,299,308,000.00 zimetolewa kwa walengwa kati ya Tsh. 3,331,728,000.00 zilizotolewa na TASAF Makao Makuu. Tsh 32,420,000.00 zimerudishwa TASAF Makao Makuu kwa walengwa hawakuweza kujitokeza kutokana na sababu mbalimbali zikiwemo vifo na kuhama katika vijiji waliyotambuliwa na kuhamia vijiji vingine.

### **MCHAKATO WA KUTAMBUA KAYA MASIKINI**

Mchakato wa kutambua kaya masikini umefanywa na wananchi kwa kushirikiana na wawezeshaji ngazi ya wilaya kwa kuzingatia vigezo vya umasikini vilivyobainishwa na mpango wa TASAF taifa. Katika mchakato huu kila kijiji kilichopo ndani ya mradi kinakua na Kamati ya usimamizi wa jamii (CMC) ambayo imepatiwa mafunzo ya utambuzi wa kaya masikini katika maeneo yao. Kamati ya CMC ikikamilisha kazi ya utambuzi wa kaya masikini inawasilisha horodha hiyo katika mkutano mkuu wa kijiji kwa ajili ya kupitishwa.

Lengo la mpango wa TASAF katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya ni kuwafikia kaya 14,195 lakini katika mchakato wa utambuzi kamati za CMC pamoja na mikutano mikuu ya vijiji imepitisha jumla ya kaya 12,075 sawa na asilimia 85 ya lengo. Lakini kutokana na mfumo wa vigezo vya kitaifa kaya 10,556 ndizo zilibainika kuwa na vigezo vya umasikini, na katika zoezi la uandikishaji kaya 10,325 kati ya kaya 10,556 zilizobainika kuwa na umasikini ndizo zilizojitokeza kujiandikisha ambapo ni sawa na asilimia 98.

### **UHAWILISHAJI FEDHA**

Utaratibu wa utoaji wa fedha unafanywa na kamati ya usimamizi wa jamii CMC iliyochaguliwa na wananchi katika kijiji husika. Kamati ya CMC inaundwa na wajumbe 14 ambao ugawanyika katika makundi mawili. Licha ya kufanya kazi ya kuchukua fedha benki na kuigawa kwa walengwa, kamati ya CMC utekeleza majukumu mengine kama

vile; kufuatilia utimizaji wa masharti kwa walengwa (kwa kufuata kalenda), kutao elimu kwa walengwa pamoja na kutunza fedha.

### **JINSI KAMATI YA CMC INAVYOFANYA KAZI**

Siku ya malipo kamati ya CMC hufika ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya kwa ajili ya kuchukua hundi ya kutolea fedha benki. Baada ya kuchukua fedha kamati hurudi kujijini kwa ajili ya kufanya malipo kwa walengwa. Fedha zinazobaki ambazo walengwa hawakujitoza kwa sababu mbalimbali kama vile kifo au kuhama, fedha hizo hurudishwa benki, na kamati husika inawasilisha hati ya kuweka fedha benki “pay in slip” Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji tayari kwa kurudishwa TASAF Makao Makuu.

### **AWAMU ZA MALIPO**

Tangu mpango huu uanze kutekelezwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya mwezi Julai 2015 hadi Februari 2017 malipo yamefanywa kwa awamu 10. Wanufaika wa mradi huu hupokea fedha kwa vipindi vya miezi miwili katika kila dirisha la malipo kwa kupokea ruzuku ya msingi na ruzuku ya masharti.